

OMBI LA KUONESHA NIA KWA UTOAJI WA WAANGALIZI WA MAMALIA NA UFUATILIAJI WA SAUTI WA BAHARINI

KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0001-00

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, unuuzi na Ujenzi wa Gati na Vifaa vya Kupakia katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu yenye uzoefu kueleza nia yao kwa:

Waangalizi wa mamalia na ufuatiliaji mwangwi na Sauti wa baharini (Passive Acoustic Monitoring-PAM).

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petrosi Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta ghafi yatapakwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufuo wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni, eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

WIGO WA VIFAA / HUDUMA:

BESIX Ballast Nedam Limited itatekeleza kwa muda wote wa mradi (Januari 2023 hadi Juni 2024) itifaki ya kupunguza athari kwa mamalia wa baharini na kelele zitokanazo na kazi ya usimikaji wa nguzo za Gati. Itifaki hii ni pamoja na:

- Utekelezaji wa uchunguzi wa mamalia wa baharini (Marine Mammal Observation - MMO) kabla na wakati wa operesheni ya kusimika nguzo
- Utekelezaji wa ufuatiliaji wa Sauti (Passive Acoustic Monitoring-PAM), Ugunduzi wa mamalia wa baharini karibu eneo la kazi.

Ili kusaidia utekelezaji wa vipengele hivi viwili, BESIX Ballast Nedam Limited inatafuta:

- Vifaa vya ufuatiliaji wa sauti (PAM equipment)
- Waangalizi wa mamalia wa baharini wenye uzoefu na waendeshaji wa

ufuatiliaji wa sauti baharini na/au

- Huduma za mafunzo ya ufuatiliaji mamalia wa baharini na uwezekano wa kufanya mafunzo kwenye kwenye eneo la mradi

KIWANGO CHA MAHTAJI:

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:

Kwa vifaa vya ufuatiliaji wa sauti (PAM equipment)

- Mbinu ya kupeleka vifaa
- Sifa za kitaalamu
- Usaidizi wa kiufundi wakati wa ufungaji vifaa na wakati wa operesheni

Kwa waangalizi wa mamalia wa baharini na waendeshaji wa vifaa vya Sauti

- CV,
- Uzoefu katika miradi kama hiyo
- Cheti cha mafunzo (ikiwezekana JNCC au kinachofanana)

Kwa huduma za mafunzo ya MMO na PAM

- CV na sifa za wakufunzi
- Mpango wa mafunzo
- Kutambulwa na mashirika ya kimataifa (JNCC au kinachowiana)
- Uwezekano wa kutoa mafunzo na kufundisha waendeshaji wadogo wa MMO / PAM kwenye eneo la kazi wakati wa ujenzi

Pia BBN itazingatia:

- Kanuni za petrosi na matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoto Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia, unashauriwa.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa procurement@bbnjv.com (Ukubwa wa Barua Pepe: MB 20 & Viambatanishi vyote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 30 Agosti 2022, Saa 6 mchana kwa saa za Tanzania.

Makampuni yanayokidhi vigezo yatatahminiwa na ikiwa yatachaguliwa, yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushirikiki katika mchakato wa zabuni.

Kumbuka: Kampuni zilizoikidhi matakwa ya mchakato wa awali wa mchujo pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni zao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.